



**WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI**



**(RITA)**

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUANZA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA USAJILI NA KUTOA VYETI VYA KUZALIWA KWA WATOTO WA UMRI CHINI YA MIAKA MITANO KATIKA MKOA WA SHINYANGA NA GEITA.**

**1. UTANGULIZI:**

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) unaendelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuhakikisha kiwango cha Usajili wa Vizazi na Vifo nchini kinaongezeka ili kuisaidia Serikali kupata takwimu sahihi za wananchi zinazoisaidia kupanga mipango ya maendeleo na huduma za jamii. Kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya mwaka **2012** ni asilimia **13.4** ya Wananchi ndiyo waliosajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo ya idadi ndogo ya Wananchi waliosajiliwa na Kupata vyeti vya kuzaliwa, Serikali kupitia RITA imeandaa maboresho ya ujumla ya mfumo mzima wa usajili chini ya Mkakati wa Kitaifa wa Kuboresha Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu [National Strategy on Civil Registration and Vital Statistics - kwa kifupi Nationa CRVS Strategy].

Mkakati wa CRVS una mipango mbalimbali ya utekelezaki ikiwa ya muda mfupi na mrefu kwa makundi yatokanayo na umri ili kufikia ufanisi unaotarajiwa. Makundi hayo ni la Watoto wa Umri **chini ya miaka mitano**, kundi la watu miaka **5 - 17** na kundi la wananchi miaka **18** na kuendelea.

Utekelezaji wa Usajili kwa kundi la kwanza umeshaanza kupitia Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano ambapo kwa sasa unatekelezwa katika Mikoa mitano ya Tanzania Bara ambayo ni Mwanza, Mbeya, Songwe, Iringa na Njombe.

Misingi ya mikuu ya Mpango huu ni:

- i. Kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wa Umri chini ya Miaka Mitano bure ikiwa lengo ni kuhakikisha watoto ambao wazazi au walezi wao hawana uwezo nao wanapata haki yao ya msingi ya kutambuliwa. Vyeti vinavyotolewa katika mpango huu vinajazwa kwa mkono na ni halali kwa matumizi yoyote.
- ii. Huduma za usajili wa watoto kusogezwa karibu na maeneo ya wananchi hivyo huduma kupatikana katika Ofisi za Watendaji kata na katika vituo vya tiba vinavyotoa huduma za afya ya mama na mtoto.
- iii. Matumizi ya teknolojia kwa kutumia simu za kiganjani katika kuchukua na kutuma taarifa kwenda katika kanzidata ya RITA hivyo kusaidia utunzaji (archiving) na upatikanaji (retrieval) wa kumbukumbu.

RITA inatekeleza Mkakati huu kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto Duniani (UNICEF), Serikali ya Canada kupitia Shirika Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo (DFATD), Kampuni ya Simu za Mkononi ya TIGO na Shirika la Wafanyakazi wa Kujitolea (VSO).

## **2. KUANZA UTEKELEZAJI KATIKA MIKOA YA SHINYANGA NA GEITA**

Tarehe 21 Machi 2017, RITA inategemea kuanza utekelezaji wa Mpango wa Usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa katika wilaya zote Wilaya tatu (3) zilizo na halmashauri 6 za Mkoa wa Shinyanga na Wilaya zote tano (5) zilizo na Halmashauri sita (6).

Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, ni asilimia **9.4** ya watoto wa Mkoa wa Shinyanga na asilimia **8.6** katika Mkoa wa Geita wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa. Lengo la RITA mara itakapoanza kutekeleza mpango huu ni kusajili watoto wote **740,912** ambao hawajasajiliwa na hawana vyeti vya kuzaliwa katika mikoa yote miwili kwa kipindi cha miezi **6**.

Ili kufanikisha utekelezaji mpango huu kutakuwa na vituo vya usajili zaidi ya **650** vitakavyokuwa na wasajili wasaidiza wapatao **1250** kwa mikoa yote miwili.

Vile vile, mafunzo tuliyoapata Mwaka jana katika utekelezaji wa mpango huu katika Mikoa ya Iringa na Njombe ambayo imeweza kusajili watoto kwa asilimia mia moja (100%) kwa kipindi cha miezi mitatu yayatumika kuhakikisha watoto wote wanapata huduma hii katika Mikoa ya Geita na Shinyanga.

## **3. HITIMISHO**

Cheti cha kuzaliwa ni nyaraka ya awali ya utambulisho kwa mtoto inayomwezesha kutambuliwa uwepo wake ambayo ni haki yake ya msingi. Kwa upande wa serikali zoezi hili ni muhimu sana kwani huiwezesha serikali kupata takwimu sahihi kuiwezesha kupanga mipango makini ya maendeleo.

Ninawaomba wadau wote ikiwa pamoja na Viongozi wa Mikoa, wilaya, halmashauri, tarafa, kata, mitaa/ vijiji na vitongoji tushirikiane kwa pamoja ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa mpango huu. Vilevile, tunawaomba Viongozi wa Dini, wanasiasa, wanahabari na viongozi wa jadi ambao watusaidia kuelimisha wananchi kuhusu kujitokeza kwa wingi kuwasajili watoto ili wapate vyeti vya kuzaliwa.

RITA tunaamini kwamba wananchi wote wa mikoa hii miwili watatumia fursa hii kuwasajili watoto ambao wana umri chini ya miaka mitano mara Utekelezaji wa Mpango huu utakapoanza rasmi.

***“Mtoto anastahili cheti cha kuzaliwa, mpe haki yake”***

**Emmy Kalomba Hudson**  
**Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu - RITA**